# PSAUMES POUR LA MESSE DE LA VEILLEE PASCALE

**COMPOSITEURS :**

Germain Lunanga Mubake

Ibrahim Bakenga

Abbé Kahumba Ambroise

Abbé Gyavira Bugandwa

Daniel Rugamika

Je viens de mettre à votre disposition, les chants des psaumes pour la veillée pascale. Les psalmodies ont été adaptées en tenant compte des syllabes muettes que contient la langue swahili et qui sont très importantes pour l'audition des textes mais ignorées par plusieurs chefs de chœurs.

Les règles de la psalmodie sont complexes et exigent un apprentissage… nombreux compositeurs autodidactes méritent une formation solide. Je tiens tout ceci lors de mes différents stages de formation en psalmodie : A l'Abbaye Notre-Dame de Tamié, Abbaye de Solesmes en France, dans le Chœur « Psalmodia » St Jean Paul II de l'Université Pontificale de Musique Sacrée de Cracovie en Pologne, et à l'Ecole du Chœur Grégorien de Paris.

Dans le cas où vous êtes intéressés à apprendre ces règles trop exigeantes, n'hésitez pas à nous contacter au +243994040363, E-mail : danielrugamikaba@yahoo.fr

Fait à Bukavu, le 10 avril 2019.

Maître Daniel RUGAMIKA B.

Membre de la Commission diocésaine de musique sacrée de l'Archidiocèse de Bukavu.

Psaume après la première lecture

# Dunia imejaa

Zaburi 32,4-5,6-7,12-13,20 na 22

Musique/ antienne: Germain LUNANGA MUBAKE
Adaptation /psalmodie: Daniel Rugamika







*cfr PH3 None TO Abbaye de la Clarté-Dieu*
*Murhesa-Archidiocèse de Bukavu RDC*

1. Neno la Bwana ni la kweli,
   matendo yake yote ni maaminifu,
   Anapenda unyofu na haki;
   dunia imejaa wema wake Bwana.

2. Mbingu zimefanywa kwa neno la Bwana,
   na jeshi lake lote kwa pumzi ya kinywa chake,
   Anakusanya maji ya baharini kama kiribani,
   anaweka vilindi mabirikani.

3. Heri taifa lenye Bwana ni Mungu wake,
   kabila alilochagua kuwa urisi wake.
   Toka mbinguni bwana anatazama,
   anaona waana wote wa watu.

4. Roho yetu inamngojea Bwana,
   Yeye ndiye msaada wetu na ngao yetu.
   Huruma yako, ee Bwana, itushukie,
   kama vile tunavyokutumainia

# UNILINDE EE MUNGU

Zaburi 15, 5 na 8, 9-10, 11
Makesha ya Paska, kisha somo la pili

Musique: IBRAHIM BAKENGA Alexandre

**Psaume après la deuxieme lecture**






1. Bwana fungu la urisi wangu na la kikombechangu :
   ndiwe unaye nilindia mali yangu.
   Namweka Bwana daima mbele ya macho yangu;
   sitatikisika, kwani yuko kuumeni kwangu.

2. Kwa hiyo moyo wangu waona furaha, nayo roho yangu yatoa shangwe,
   hata mwili wangu utapumzika salama.
   Kwani hutaiacha roho yangu kuzimuni,
   wala hutamkubali mwamini wakoaingie shimoni.

3. Utanionyesha njia ya uzima,
   wingi wa furaha mbele ya uso wako,
   anasa za milele
   kuumeni kwako.

Fit à la Cathédrale NDPaix/Bukavu 2014
ibrahimbakengaalexandre@gmail.com

Psaume après la 3ème lecture

# Tumwibie Bwana

**( kutoka15,1-18)**

**A.KAHUMBA Ambroise**







2. Bwana Mungu wetu ni Muhodari wa vita
   magari ya Farao yamefunikizwa
3. Wateule wa Farao na jeshi lake
   walizama majini mwa bahari ya Sham
4. Mkono wako wa kuume umejivika
   umevunja adui, umewavunja

# ENYI MATAIFA.

Zab 29, 2 na 4, 5-6,11-12 na 13b

Psaume après la 4ème lecture

Musique: A. Gyavira BUGANDWA
Adaptation psalmodie: Daniel Rugamika










1. Nakutukuza, ee Bwana, kwa kuwa umeniokoa
   wala hukuwafurahisha adui zangu juu yangu
   Ee Bwana, umeondoa roho yangu kuzimuni,
   Umeniokoa katika wale wanaoshuka shimoni.

2. Mwimbieni Bwana, enyi waamini wake,
   Shukuruni jina lake takatifu.
   Kwani hasira yake ni kitambo kidogo,
   mapendo yake yadumu maisha yote.

3. Usikie, ee Bwana, unihurumie,
   ee Bwana, uwe msaada wangu.
   Umegeuza kilio changu kuwa mchezo,
   ee Bwana, mungu wangu, nitakusifu milele.

Psaume après la 5ème lecture

# Mtachota maji

Is 12, 2-3,4bcd, 5-6

Daniel Rugamika B.







*Ton Boquen cfr Abbaye de la Clarté-Dieu*
*Murhesa-Bukavu RDC*

1. Sasa Mungu ni Mwokozi wangu,
   namtumainia, wala sina hofu tena.
   kwa kuwa Bwana ni nguvu yangu na wimbo wangu
   Bwana amekuwa wokovu wangu.

2. Nanyi mtachota maji kwa furaha/ visimani mwa wokovu.
   Mtukuzeni Bwana, liombeni jina lake,
   tangazeni matendo yake kati ya mataifa,
   wakumbusheni ya kuwa jina lake ni tukufu.

3. Mwimbieni Bwana, maana ametenda makuu,
   nayo yatangazwe duniani kote.
   Pigeni kelele za furaha na shangwe, wenyeji wa Sioni,
   maana ametukuzwa ndani yenu mtakatifu wa israeli.

# Ee Bwana, wewe unayo maneno.

Psaume après la 6ème lecture

zab.18,8,9,10,11.

Daniel Rugamika B.







*Chd Eolien 7.cf abbaye de la Clarté-Dieu*
*Murhesa- Bukavu RDC*

1.Sheria ya Bwana ni kamilifu,
yatuliza roho
mafundisho ya Bwana ni imara,
yamletea mjinga elimu.

2. Amri za Bwana ni za haki,
zafurahisha moyo;
agizo la Bwana ni safi,
layatia macho mwangaza.

3. Ibada kwa Bwana ni safi,
yadumu hata milele;
hukumu za Bwana ni kweli,
zote za haki kamili

4. Zatamanika kuliko zahabu,
kuliko wingi wa zahabu safi;
ni tamu kuliko asali,
kuliko mavuno ya uki.

Psaume après la 7ème lecture

# Uniumbie moyo safi

Zaburi 50,12-13,14-15,18-19.

Germain Lunanga Mubake




1. Uniumbie moyo safi, ee Mungu,
   utengeneze tena ndani yangu roho imara
2. Usinitupe mbali na uso wako,
   wala usiniondoshee roho yako takatifu.
3. Unirudishie furaha ya wokovu wako,
   unisabitishie roho karimu
4. Nitawafundisha waasi njia zako,
   nao wakosefu watakuongekea
5. Kwa maana hupendezwi na sadaka
   ningetoa sadaka ya kuteketezwa,/ hungeipokea;
6. Sadaka yangu, ee Mungu, ni roho ya kutubu:
   moyo uliotubu na kupondeka/, ee Mungu, hutazarau.